# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA MITAA

## MKOA WA DAR ES SALAAM

## HALMASHAURI YA MANISPAAA YA KIGAMBONI

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA WILAYA YA KIGAMBONI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI

## WAKATI WA ZIARA YAKE WILAYANI KIGAMBONI TAREHE 11 FEBRUARI 2020

**OFISI YA MKUU WA WILAYA**
**S. L. P 36124**
**KIGAMBONI**
**DAR ES SALAAM**

**FEBRUARI, 2020**

**WILAYA YA KIGAMBONI**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO ZA SERIKALI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DR. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI KIPINDI CHA KUISHIA JANUARI 2020

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya ya Kigamboni ni moja kati ya Wilaya **5** zinazounda Mkoa wa Dar es Salaam. Wilaya ya Kigamboni ilianzishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 462 la mwaka 2015 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi karibu zaidi.

## ENEO LA WILAYA

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya ya Kigamboni ina eneo la kilomita za mraba 577.9 sawa na hekta 57,786.8 na ukanda wa Pwani wenye urefu wa kilometa 65. Aidha Wilaya ya Kigamboni kwa upande wa mashariki inapakana na Bahari ya Hindi, kusini inapakana na Wilaya ya Mkuranga – Mkoa wa Pwani na upande wa kaskazini inapakana na Bahari ya Hindi na upande wa magharibi imepakana na Wilaya ya Temeke.

## IDADI YA WATU

**Mheshimiwa Rais;**

Kufuatia Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Wilaya ya Kigamboni ilikuwa na jumla ya watu **162,932** na kaya **40,133.** Kati ya hao wanaume walikuwa **81,199** na wanawake walikuwa **81,733**. Hadi kufikia Desemba mwaka 2019, Wilaya ya Kigamboni inakisiwa kuwa na wakazi wapatoa **238,591** kati yao wanawake ni **119,686** na wanaume ni **118,905** hii ni kutokana na ongezeko la asilimia 5.6 kwa mwaka.

## UTAWALA

**Mheshimiwa Rais;**

Kiutawala Wilaya ya Kigamboni ina Tarafa 3, Kata 9, Mitaa 67, Jimbo 1 la uchaguzi na Baraza la Madiwani lenye wajumbe 15 ambao tisa (9) ni wa kuchaguliwa na wanne (4) ni wa viti maalum.

**Mheshimiwa Rais;**

Tunaishukuru Serikali yako ya awamu ya tano kwa Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni – Gezaulole. Mpaka sasa jumla ya Shilingi 4,300,000,000.00 zimepokelewa kati ya Shilingi 5,276,842,700.00 kutoka Serikali Kuu na ujenzi upo hatua za ukamilishaji kupitia mkandarasi TBA kwa gharama ya Shilingi 5,113,690,000.00 na Meneja wa mradi Chuo kikuu Ardhi kwa Shilingi 163,152,700.00 na jengo limeanza kutumika.

Pia Kuanza kwa ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Gezaulole, hadi sasa ujenzi upo hatua za awali za utekelezaji. Jumla ya Shilingi 63,167,550.00 zimetolewa kutoka Mapato ya Ndani kwa utekelezaji huu kupitia “Force Account”.

Vile vile Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni - Gezaulole, upo hatua za ukamilishaji kupitia Mkandarasi TBA kwa Mkataba wa Shilingi 1,618,149,133.00. Mpaka sasa jumla ya Shilingi 1,202,493,727.00 zimepokelewa toka Serikali Kuu na kutumika. Mradi huu unasimamiwa moja kwa moja na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa kwa Kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa na sasa jengo hili limeanza kutumika.

Aidha, utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Tarafa ya Somangila kwa Shilingi 150,000,000.00 umekamilika.

## AFYA

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya ya Kigamboni ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 31 ambapo kati ya hivyo 19 ni vya Serikali na 12 ni vya binafsi, kati ya hivyo Hospitali ni moja(1), vituo vya afya vinne(4) na zahanati ishirini na sita (26) vinavyotoa huduma kwa wakazi wa Wilaya ya Kigamboni na maeneo ya jirani.

Kituo cha Afya Vijibweni ndiyo hutoa huduma za Afya kama Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni, ambayo inahudumia wagonjwa kati ya 150 hadi 200 kwa siku.

Katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba "**kila Kijiji kuwa na Zahanati, kila Kata kuwa na Kituo cha Afya na Wilaya kuwa na Hospitali**" Wilaya ya Kigamboni imefanikiwa kujenga na kukamilisha Zahanati **3** za Buyuni, Kijaka na Pembamnazi zilizojengwa kwa gharama ya **Shilingi. 265,616,680.20.** Upanuzi wa Vituo vya Afya **2** vya Kigamboni na Kimbiji umefanyika kwa gharama ya **Shilingi. 914,429,385.00** ambazo Serikali Kuu imetoa Shilingi 800,000,000 kwa mgawo wa Shilingi 400,000,000 kila Kituo, na Mapato ya Ndani Shilingi 114,429,385.00. Huduma za Upasuaji, Maabara, Wodi ya Wazazi na Chumba cha kuhifadhia maiti zinatolewa.

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni, jumla ya **Shilingi. 1,500,000,000.00** zimepokelewa na majengo yote saba ya awali (Jengo la Utawala, Famasia, Kufulia, Wagonjwa wa Nje, Maabara, Mionzi na Wazazi) yapo hatua za umaliziaji kwa asilimia 93 ya ujenzi kwa awamu ya kwanza. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 tunatarajia kupokea fedha kiasi cha Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kuongeza majengo mengine.

Ujenzi wa Jengo la Uchunguzi Kituo cha Afya Vijibweni na ukarabati wa majengo matano ya Zahanati za Kibada, Mbutu na Pembamnazi umetekelezeka kwa gharama za **Shilingi. 351,000,000.00**

Aidha, ununuzi wa vifaa tiba na vitendanishi kama X-rays mashine 2 na Ultra sound 1 zenye thamani ya **Shilingi. 386,000,000.00** umefanyika kwa Vituo vya Afya Vijibweni na Kigamboni.

Mbali na uboreshaji wa miundombinu ya Afya, jumla ya **Shilingi. 458,892,000.00** zimepokelewa katika jitihada nzima ya uboreshaji wa huduma za afya kupitia fedha za Mfuko wa Pamoja (HSBF) za uboreshaji huduma, ununuzi wa Dawa na vifaa tiba na **Shilingi. 936,068,296.48** pia za ununuzi wa dawa, vifaa tiba toka bohari kuu ya dawa MSD na **Shilingi. 57,800,000.00** za ununuzi wa dawa za chanjo kwa kipindi cha kuanzia 2016/2017 hadi 2018/2019.

Maboresho ya huduma yamefanyika Hospitali ya Vijibweni ambapo jengo la uchunguzi wa Mionzi limejengwa kwa thamani ya **Shilingi.101,000,000.00** na mashine ya X-ray yenye thamani ya **Shilingi. 157,000,000.00** ambapo jengo limekamilika. Gharama za ujenzi pamoja na Mashine ya X-ray zinatokana na mkopo kutoka BIMA ya Afya. Pia katika Kituo cha Afya Kigamboni,

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imefanikiwa kununua mashine za kisasa za mionzi (X ray) kwa **Sh.174,000,000.00** ikiwa ni mkopo kutoka Mfuko wa Bima ya Afya na Mashine ya "Ultra Sound"kwa **Shilingi.55,000,000.00** kwa fedha za mapato ya ndani.

**ELIMU YA MSINGI**

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya ya Kigamboni ina jumla ya shule za Msingi **57,** kati ya hizo shule **33** ni za Serikali na shule **24** zisizo za serikali. Shule hizi zina jumla ya wanafunzi **40,077** miongoni mwao wanafunzi **33,316** ni wa shule za Serikali na wanafunzi **6,761** ni wa shule za binafsi.

Kitaaluma Wilaya ya Kigamboni inafanya vizuri kwa kipindi hiki cha Miaka mitatu kama inavyojifafanua kwenye jedwali lifuatalo;-

| Mwaka | Waliosajiliwa | | | Waliofanya | | | Waliofaulu | | | % ya ufaulu | Nafasi | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wav | Was | Jml | Wav | Was | Jml | Wav | Was | Jml | | Mkoa | Taifa |
| 2017 | 1,475 | 1,608 | 3,083 | 1,471 | 1,606 | 3,077 | 1,371 | 1,432 | 2,803 | **91.1** | **3** | **7** |
| 2018 | 1,679 | 1,788 | 3,467 | 1,670 | 1,778 | 3,448 | 1,572 | 1,608 | 3,180 | **92.2** | **3** | **10** |
| 2019 | 1,868 | 1,898 | 3,766 | 1,843 | 1,887 | 3,730 | 1,739 | 1,729 | 3,468 | **92.98** | **3** | **19** |

**Mheshimiwa Rais;**

Katika kipindi cha Miaka mitano ya Serikali tumepata mafanikio mengi ikiwemo ujenzi wa madarasa 56 na ukarabati wa madarasa 15 kwa jumla ya Shilingi 831,475,853.00, katika Shule za Msingi Bohari, Mikenge, Kisota, Muhimbili, Kijaka, Mkundi, Raha leo, Gomvu, Kisarawe II, Chekeni Mwasonga, Vijibweni, Kisiwani na Mkamba.

Jumla ya matundu ya vyoo **125** yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi. 423,261,700.00** katika Shule za Msingi Kibugumo, Buyuni, Kichangani, Mikenge, Mkundi, Kigogo, Pembamnazi na Mwongozo.

Ununuzi wa madawati **3,470** yenye thamani ya **Shilingi. 416,400,000.00**. Ujenzi wa nyumba 2 za walimu katika Shule za Msingi Kijaka na Vumilia Ukooni zimejengwa kwa gharama ya **Shilingi. 132,758,861.48**

Mafanikio mengine ni mapokezi ya fedha za Elimu Bure **Shilingi 929,577,304.11** na **Shilingis 351,275,440.40** kutoka Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) kwa ajili ya uendeshaji wa Shule za Msingi.

**ELIMU YA SEKONDARI**

**Mheshimiwa Rais;**

Halmashauri ya Manispaa Kigamboni ina jumla ya shule za Sekondari 22, kati ya hizo 15 ni za Serikali na 7 za Binafsi. Aidha, zipo shule 4 za Serikali zenye bweni ikiwemo Kimbiji, Kisarawe II, Pembamnazi na Nguva yenye kidato cha tano na sita.

**Mheshimiwa Rais;**

Serikali ya awamu ya tano imewezesha upatikanaji wa Elimu bure ya Sekondari, jumla ya **Shilingi. 505,407,265.30** toka fedha za EP4R na **Shilingi. 2,186,029,192.68** toka ruzuku ya elimu bure Serikali Kuu zilipokelewa ambapo madarasa **22** yamejengwa na madarasa **71** kukarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi. 526,869,392.59** katika sekondari za Kisota, Nguva, Kigamboni, Aboud Jumbe, Pemba mnazi, Kisarawe II na Kibada.

Jumla ya **Shilingi 26,552,327.00** zimetumika katika ukarabati wa maabara Sekondari ya Aboud Jumbe na **Shilingi. 262,500,000.00** zimepokelewa kama ruzuku maalumu ya ukamilishaji wa miradi viporo (Maboma) kwa sekondari za Nguva, Vijibweni, Kibada na Kigamboni. Ujenzi wa mabwalo ya chakula **3** kwa gharama za **Shilingi. 310,000,000.00** kwa sekondari za Nguva, Kisarawe II na Pembamnazi.

Ujenzi ya mabweni **3** na kununua vitanda 100 kwa **Shilingi. 334,000,000.00** Sekondari ya Nguva (2) na Kisarawe II (1)

Ujenzi wa majengo **3** ya utawala katika Sekondari za Nguva, Kisarawe II na Pembamnazi. Vile vile umefanyika Ujenzi wa nyumba **2** za walimu (6 kwa 1) kwa gharama ya **Shilingi 448,315,060.00**, Ununuzi wa madawati **1,403** kwa gharama ya **Shilingi 229,562,000.00** na Ujenzi wa matundu ya vyoo 86 kwa gharama ya **Shilingi 377,394,899.00** katika Shule za Sekondari za Aboud Jumbe, Kisota, Vijibweni, Pembamnazi, Kimbiji, Kibada, Kisarawe-II na Nguva.

**UJENZI NA BARABARA**

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya ina mtandao wa barabara zenye urefu wa km **1025.94**. Kati ya hizo km 48.64 ni za lami, km 413.47 ni za changarawe na km 563.86 ni za udongo. Barabara zilizopo chini ya TARURA ni km. 883.05 (86.1%) na zilizo chini ya TANROADS ni km 142.89 (13.9%).

Barabara ya Tungi – Kibada yenye urefu wa Km 3.8 inaendelea kwa asilimia 50 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 7.6. Barabara za Mji Mwema – Cheka – Pembamnazi yenye Km 38 kwa Shilingi Billioni 30 na Kibada – Mwasonga – Kijaka – Kimbiji yenye Km 48 kwa Shilingi Billion 60 zinasubiria kibali kwa ajili ya kutangaza zabuni.

Kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Ibara Na. 38 – 41 inaelekeza uboreshwaji wa miundo mbinu ya barabara, katika kutekeleza hilo Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Manispaa ya Kigamboni imejenga jumla ya km 1.81 kwa kiwango cha lami, haya ni mafanikio makubwa sana kwa Wilaya kwani hapakuwa na Barabara hata moja ya kiwango cha lami iliyo chini ya Wilaya.

Pia, Halmashauri kwa sasa kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imeweza kusajili na kuhakiki upya Mtandao wa Barabara za Manispaa ya Kigamboni katika mfumo wa "satellite" kupitia "DROMAS" na kuongezeka hadi kufikia kilomita za barabara **883.05** na kufanya mfumo wa barabara wa Kigamboni kutambulika kote duniani.

Kumekuwa na ushirikiano mzuri kati ya Halmashauri na TARURA katika utekelezaji wa mipango ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, aidha Halmashauri imefanikisha ujenzi wa barabara ya Kijaka – Mwasonga yenye urefu wa km 8.1 kwa gharama ya **Shilingi. 174,000,000.00** kwa kiwango cha Changarawe. Barabara hii ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa kiuchumi katika Wilaya ya Kigamboni kwani imefungua njia ya mawasiliano kutoka Kata ya Kimbiji kuliko na kiwanda cha saruji na kata ya Kisarawe II.

**MAJI**

**Mheshimiwa Rais;**

Katika kukabiliana na upungufu wa maji na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maji safi na salama, Wilaya ya Kigamboni kupitia DAWASA imeanza kutekeleza mradi kupitia Mkandarasi Advent Construction Company kwa muda wa miezi 15 kuanzia Desemba 2019 hadi Machi 2021 kwa gharama ya Shilingi 10,000,000,000.00.

Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa Tanki kubwa la ujazo wa lita 15,000,000, ujenzi wa kituo cha kusukumia maji, ujenzi wa bomba kubwa la kusafirishia maji pamoja na kuendeleza visima 8 kati ya visima 20. Mpaka sasa Mkandarasi yupo ''site'' anaendelea na kazi.

Vile vile, Wilaya ya Kigamboni inatekeleza mradi wa usambazaji maji Mtaa wa Chambewa Kata Pembamnazi ambapo hadi kukamilika kwake utagharimu **Shilingi. 134,535,500.00** na hadi sasa mradi upo asilimia 70% kupitia Mkandarasi Syscon Builders.

Serikali inatekeleza miradi ya usambazaji maji Mtaa wa Malimbika Kata ya Somangila na Kibene Kata ya Vijibweni ambapo hadi kukamilika kwake itagharimu **Shilingi. 679,804,900.00** na hadi sasa mradi upo asilimia 40%

## MAENDELEO YA JAMII NA VIJANA

**Mheshimiwa Rais;**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni inatekeleza agizo la Serikali kwa kutenga 10% ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo **isiyo na riba** kwa vikundi vya wajasiliamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Hadi sasa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni tangia kuanzishwa kwake imekwisha toa mikopo yenye thamani ya **Shilingi 1,120,344,600.00 (**Bilioni moja milioni mia moja ishirini laki tatu na arobaini na nne elfu na mia sita**),** kwenye vikundi **372** vyenye jumla ya wanufaika **2,875**.

Muhtasari wa mikopo yote iliyotolewa.

| Mwaka wa fedha | Fedha zilizotolewa | Makundi nufaika | Idadi ya vikundi | Idadi ya wanufaika | Kiasi kwa kila kundi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 88,950,600 | Wanawake | 23 | 575 | 45,000,000 |
| | | Vijana | 12 | 60 | 43,950,600 |
| **Jumla** | | | **45** | **635** | **88,950,600** |
| | | | | | |
| 2017/2018 | 231,394,000 | Wanawake | 19 | 95 | 49,894,000 |
| | | Vijana | 76 | 380 | 181,500,000 |
| **Jumla** | | | **95** | **475** | **231,394,000** |
| | | | | | |
| 2018/2019 | 500,000,000 | Wanawake | 92 | 460 | 228,500,000 |
| | | Vijana | 54 | 410 | 228,010,000 |
| | | walemavu | 8 | 40 | 43,490,000 |
| **jumla** | | | **154** | **910** | **500,000,000** |
| | | | | | |
| 2019/2020 | 300,000,000 | Wanawake | 66 | 660 | 208,000,000 |
| Julai-sept | | Vijana | 21 | 210 | 88,500,000 |
| | | walemavu | 1 | 5 | 3,500,000 |
| **jumla** | | | **88** | **875** | **300,000,000** |
| | | | | | |
| **JUMLA KUU** | | | **372** | **2895** | **1,120,344,600** |

**USAFI NA MAZINGIRA:**

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya ya Kigamboni inatekeleza majukumu ya kusafisha na kuhifadhi mazingira kwa kuwashirikisha wananchi na wadau mbali mbali.

Kiwango cha uzalishaji wa taka kwa siku katika Manispaa ya Kigamboni ni tani 228 kwa siku. Kati ya hizo, Halmashauri ina uwezo wa kudhibiti tani 147 (64.7%) kwa siku. Uhamasishaji unaendelea kwa kushirikisha jamii na vikundi vya vijana na akina mama katika usafishaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali. Wilaya katika kuhakikisha inasimamia usafi wa mazingira imebinafsisha kazi za uzoaji na ukusanyaji wa taka kwa vikundi vya kijamii na wakandarasi katika ngazi ya Kata na kazi hiyo inaendelea chini ya usimamizi wa Halmashauri kupitia Idara ya Mazingira na udhibiti wa taka ngumu.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni iko katika mpango wa kuanzisha dampo la kisasa eneo la Lingato – Kisarawe-II kwa ajili ya kutupa taka ngumu kwa matumizi ya jiji la Dar es salaam. Eneo kwa ajili ya uanzishaji wa dampo hili limepatikana katika Mtaa wa Lingato Kata ya Kisarawe II, kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ibara ya 80. Hii inatokana na gharama kubwa zaidi katika kivuko cha Ferry na Daraja la Mwl Nyerere.

**MIFUGO NA UVUVI:**

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya imeendelea kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi kupitia ibara ya 23 hadi 26 kwa shughuli mbali mbali za uboreshwaji wa huduma za mifugo na uvuvi zikiwemo za ushauri wa mbinu bora za uzalishaji, kinga na tiba dhidi ya magonjwa mbalimbali na udhibiti wa uvuvi haramu.

Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka 2019/2020 katika kutambua idadi ya wavuvi waliopo ndani ya Manispaa, ilianzisha utaratibu wa utoaji wa leseni, doria na kusajili vyombo vya uvuvi ambapo jumla ya leseni 1,333 zilitolewa kwa vyombo 423 ambapo Boti ni 85, Ngwanda 34, Dau 23, Mitumbwi 225, Mashua 6 na Ngalawa 50. Hii imeleta tija kwani sasa wavuvi wanajulikana na imepunguza uvuvi haramu.

Katika kupambana na uvuvi haramu, Manispaa ina BMU's 17 katika ukanda wa bahari ambao wanadhibiti uvuvi haramu wakishirikiana na wataalam pamoja na Jeshi la polisi la Maji (Marine Police)

Katika Sekta ya Mifugo, Wilaya iliweza kutoa ushauri kwa wafugaji **6,641** na kutoa kinga na tiba dhidi ya magonjwa mbalimbali kwa wanyama **101,676** wakiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, mbwa, nguruwe na kuku. Pia uhimilishaji ulifanyika kwa ng'ombe 77 na ndama waliozaliwa ni **4,625**.

## KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA.

**Mheshimiwa Rais;**

Wakulima 2,845 katika Wilaya walipata ushauri juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu na mbolea katika mazao ya mboga, matunda na nafaka. Mafunzo kwa wakulima mashambani (onsite training) yalitolewa kwa wakulima 6,675 (61%) kati ya wakulima 10,859, kutokana na mafunzo na ushauri tija ya uzalishaji wa mazao mbalimbali imeongezeka kutoka wastani wa tani 0.8 hadi tani 3.0 katika mazao ya bustani, na kutoka tani 4.0 - 6.0 zao la muhogo, tani 0.5 - 1.8 zao la mpunga na tani 4.0 - 6.0 zao la viazi vitamu.

Ongezeko hili limetokana na wakulima kuzingatia elimu ya matumizi ya mbegu bora, utaalam wa matumizi sahihi ya nafasi katika kupanda mazao ikiwa pia ni utekelezani wa ilani kupitia ibara ya 21 hadi 22. Kila Kata ina shamba darasa linalotumika kutoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo.

Jumla ya wanachi 250 wamepatiwa elimu ya ujasiliamali kwenye Nyanja za kilimo, mifugo na masoko.

## MIPANGO MIJI NA ARDHI

**Mheshimiwa Rais;**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa kutambua umuhimu wa kupanga mji kwa matumizi sahihi ya ardhi na kupunguza makazi holela imefanya yafatayo;

1) Jumla ya viwanja **7,123** ambavyo vimepimwa katika Manispaa ya Kigamboni kwa ushirikiano wa Manispaa na Makampuni ya upimaji na viwanja vinavyoendelea kupimwa chini ya mpango wa urasilimishaji jumla ya viwanja 9,111. Jumla ya hati miliki 2,000 za viwanja za kawaida zimetolewa kwa wananchi.

2) Jumla ya hekta 4,015 zimepimwa sawa na ekari 10,037.5
3) Jumla ya michoro 235 ya Mipangomiji imeandaliwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo viwanja vya makazi, na viwanda
4) Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imeshiriki kikamilifu katika maandalizi ya Mpango Kabambe(Master Plan) na kwa sasa tupo hatua za mwisho wa kuandaa Mpango kina wa utekelezaji "kigamboni Details Plan Framework and Guideline ambao utaongoza kutekeleza mpango kabambe wa Dar es salaam na Kigamboni.
5) Masijala ya Ardhi imeanzishwa

Halmashauri katika kutatua Migogoro ya ardhi na kuthibiti ongezeko la malalamiko ya ardhi iliamua kufanya yafatayo;

1) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya sheria za Ardhi na mipango miji, ambapo mikutano ya wananchi imefanyika katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kigamboni, kueleimisha umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.
2) Jumla ya mabaraza ya ardhi ya kata 9 yameanzishwa na yanasaidia kutatua migogoro
3) Jumla ya wataalamu 10 walipewa mafunzo ya upimaji ardhi wa kisasa ambapo Halmashauri kupitia fedha za ndani imefanikiwa kununua vifaa vya kisasa vya upimaji ( GPS RTK) kwa Shilingi 69,000,000.00

Kwa ushirikiano na makampuni binafsi na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, upimaji wa viwanja kwa ajili ya makazi na viwanda umeendelea kufanyika ili kuifanya Halmashauri ya Kigamboni kuwa ya mfano katika Jiji la Dar es Salaam.

Katika kuitikia wito wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa viwanda, jumla ya viwanja **456** vimepimwa kwa ajili ya viwanda katika eneo la KisaraweII.

## FEDHA NA BIASHARA

**Mheshimiwa Rais;**

Wilaya imeendelea kuboresha mfumo wa ukasanyaji wa mapato, ili kuweza kupata fedha za kuwahudumia wananchi kupitia huduma na miradi mbalimbali, katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa Halmashauri iliweza kufanya yafatayo;

1) Kufunga mifumo ya kielektroniki ya kukusanyia mapato (LGRCS) ambayo imeongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani
2) Kukusanya mapato kwa kushirikisha idara zote za Manispaa
3) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi na ushuru mbalimbali kwa maendeleo yao

Kwa upande wa mapato ya ndani, Halmashauri inaendelea kuboresha makusanyo kwa kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha Shilingis 8,223,571,540.00 na kufanikiwa kukusanya Shilingi 2,923,666,731.00 sawa na asilimia 36 ya mapato halisi.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha Shilingis 9,218,868,000.00 na makusanyo halisi yalikuwa Shilingi 5,004,065,028.00 sawa na asilimia 54, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha Shilingis 8,671,113,000.00 na makusanyo halisi yalikuwa Shilingi 6,997,652,939.00 sawa na asilimia 81 na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mpaka Halmashauri tumekisia kukusanya Mapato ya Shilingi 5,686,970,688.00 na hadi kufikia tarehe 9 Februari 2020 Halmashauri imekusanya kiasi cha Shilingis 3,812,479,643.00 sawa na asilimia 68.09.

Vile vile tunategemea Mapato kuongezeka zaidi mara baada ya Mradi wa Kimkakati wa Soko la Kimataifa – Kibada kukamilika Mwaka 2020/2021 na kuanza kutumika kwa wafanyabiashara zaidi ya 320. Mradi huu wenye thamani ya Shilingis 13,030,384,450.66 kupitia Mkandarasi MECCO na hadi sasa upo hatua ya kumimina zege la msingi na kupandisha kuta sakafu ya ardhi (ground floor)

## UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2019

**Mheshimiwa Rais;**

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019, Hamashauri ya Manispaa ya Kigamboni kama zilivyo Hlmashauri zingine nchini zilifanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa tarehe 24/11/2019 Katika mitaa yote 67. Uchaguzi huu ulifanyika kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa za mwaka 2019 na tangazo la Serikali Na. 372 la tarehe 26/4/2019. Viongozi waliochaguliwa ni pamoja na

1. Wenyeviti wa Serikali za mitaa, na
2. Wajumbe wa Serikali za Mitaaa.

Halmashauri ilitarajia kuandikisha jumla ya wapiga kura 112,244 kati ya hao wanaume ni 55,294 na wanawake 56,950. Hadi kufikia mwisho wa zoezi la uandikishaji jumla ya wapiga 90,296 waliandikishwa sawa na asilimia 80.4.

Jumla ya vyama 9 vya siasa vilishiriki uchaguzi kwa kufuata kanuni na miongozo iliyotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Chama cha Mapinduzi (CCM) kilipata **ushindi wa asilimia 100** kwa kupata wenyeviti 67 na wajumbe wa Serikali za Mitaa 337

## CHANGAMOTO ZA WILAYA YA KIGAMBONI

**Mheshimiwa Rais;**

Changamoto zinazoikabili Wilaya ya Kigamboni ni pamoja na hizi zifuatazo;-

1. Uhaba wa maeneo ya uanzishwaji wa Taasisi za Serikali hasa Shule za Msingi kama ilivyo Vijibweni yenye wanafunzi wengi zaidi na kuhitaji shule nyingine mpya,
2. Kutokuwa na walimu wa kutosha hasa masomo ya hisabati na sayansi hali inayopelekea wanafunzi wengi kufeli masomo hayo na kusababisha ukosefu wa wataalam katika kada za masomo ya sayansi kama vile udaktari n.k.
3. Uhaba wa vitendea kazi vya usimamizi wa miradi na usafi wa mazingira hasa magari ya kubeba taka ngumu, magari ya miradi na ukusanyaji wa mapato,
4. Mwitikio mdogo wa wananchi katika ulipaji wa Ushuru na kodi mbalimbali,
5. Wananchi kutojitokeza kumilikisha ardhi yao baada ya upimaji,

## MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WILAYA YA KIGAMBONI

**Mheshimiwa Rais;**

1. Wilaya itaendelea kuongeza bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya Elimu, Afya, Maji na Usafishaji ili kuimarisha utoaji wa huduma, pamoja na kuendelea kuomba maeneo ambayo hayajatumika kwa muda mrefu likiwemo eneo la NSSF,

2. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya sheria mbalimbali zinazohusu tozo na kodi mbalimbali na umuhimu wake.
3. Kushirikisha wadau mbalimbali katika upimaji wa ardhi na uendelezaji wa ardhi ndani ya Wilaya ya Kigamboni,
4. Kuendelea kuomba nafasi za ajira kupitia bajeti zetu ili kukabiliana na upungufu wa walimu na watumishi wa kada mbalimbali,
5. Kuendelea kupima maeneo mbalimbali ili kupanga mji wetu na kuondoa kero mbalimbali zilizopo.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Rais;**

Kwa taarifa hii naomba nikukaribishe Wilayani Kigamboni ili utembelee, ukague utekelezaji wa shughuli za Serikali na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na tupo tayari kukusikiliza ili utushauri na kutupa maelekezo ya Serikali na tupo tayari kuyatekeleza ili kuweza kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Rais;**

**KARIBU SANA KIGAMBONI**

**SARA MSAFIRI ALLY**
**MKUU WA WILAYA**
**WILAYA YA KIGAMBONI**